

Nafasi ya Kiswahili katika Utoaji wa Huduma za Afya Tanzania

Adventina Buberwa
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ikisiri

Lugha ya Kiswahili kama zilivyo lugha nyingine duniani, hufanikisha mawasiliano katika jamii. Mawasiliano hayo yanaweza kuwa ya watu wa utamaduni mmoja au watu wa jumuiya kubwa zenye wazungumzaji wa lugha mbalimbali na wenye tamaduni tofauti. Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na jamii kubwa zaidi Afrika Mashariki hususan Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Kongo na kwingineko (Kiango, 2002). Lengo la makala haya si kujadili nafasi ya Kiswahili kwa mwelekeo wa mawanda hayo mapana, bali kujielekeza katika eneo mahususi ili kubainisha na kujadili nafasi ya Kiswahili katika utoaji wa huduma za afya nchini Tanzania. Makala haya yanazingatia kuwa licha ya lugha ya Kiswahili kuwa lugha inayofahamika sana kwa Watanzania waliowengi, zipo changamoto mbalimbali zinazowakabili Watanzania wanapotumia lugha ya Kiswahili wakati wa kutoa au kupokea huduma za afya nchini. Changamoto hizi ni pamoja na wataalamu wa afya kupata mafunzo kwa lugha za kigeni suala linalosababisha wataalamu hao kukosa msamiati wa kitaalamu wa lugha ya Kiswahili, matumizi ya lahaja mbalimbali za Kiswahili, kutofautiana kwa lugha mama na tamaduni za lugha husika na matumizi ya misimu au lugha za mitaani. Kutokana na changamoto hizi, lugha ya Kiswahili hushindwa kutumika kikamilifu katika mawasiliano baina ya watoaji na wapokeaji wa huduma za afya.

Maneno Muhimu: Huduma za afya, Kiswahili, Tanzania

Utangulizi

Sayansi na teknolojia kutoka katika nchi za Magharibi imekuja Afrika kupitia katika lugha za kigeni hususani lugha ya Kingereza (King'ei, 1999). Lugha hii imekuwa ikitumika kama lugha rasmi na wakati mwingine kama lugha ya taifa katika baadhi ya nchi za Kiafrika hususani Afrika Mashariki. Kwa mfano, lugha ya Kingereza ni lugha rasmi ya mawasiliano katika nchi za Tanzania, Kenya na

Uganda. Aidha, nchini Tanzania, lugha ya Kingereza imekuwa ikitumika kama lugha ya kufundishia katika baadhi ya ngazi za elimu zikiwemo ngazi ya elimu ya msingi¹, sekondari, vyuoni hata katika ufundishaji wa elimu ya juu. Kutokana na hali hiyo, vitabu vingi na machapisho vimeandikwa kwa lugha ya Kingereza suala ambalo husababisha wanafunzi wa nchi za Afrika kusoma machapicho yaliyoandikwa kwa lugha hiyo. Kwa hiyo, lugha ya Kingereza imeifanya lugha ya Kiswahili kukosa nafasi ya kukua na kuendelea kikamilifu katika nyanja mbalimbali hususani katika uga wa sayansi (Mazrui na Mazrui, 1995).

Kutokana na matumizi ya lugha za kigeni katika ufundishaji na ujifunzaji, lugha nyingi za Kiafrika ama zimekosa nafasi au kupata nafasi finyu za kuteuliwa kuwa miongoni mwa lugha za kufundishia suala ambalo limekuwa likidumaza lugha za Kiafrika. Kutokana na ufinyu huo wa kimatumizi, lugha nyingi za kiafrika ama hazina au zina istilahi chache za kisayansi zinazofahamika.

Tofauti na lugha zingine za Kiafrika, Kiswahili ni lugha ambayo imekuwa ikiendelezwa na kukuzwa kwa jitihada kubwa. Istilahi mbalimbali zimekuwa zikiundwa kutokana na jitihada za taasisi mbalimbali zikiwemo Taasisi ya Taaluma za Kiswahili² (TATAKI) na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA). Kwa miaka ya hivi karibuni matumizi ya lugha hii yameongezeka sana. Lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumika katika nyanja mbalimbali nchini Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla. Lugha hii hutumika katika muziki, siasa, kazini, kwenye shughuli za kidini, katika vyombo vya habari na shughuli za kijamii nyinginezo (Mukuthuria, 2006; Moshi, 2006; Habwe, 2009;). Kiswahili kimepunguza tofauti na kuleta umoja ama wa kitaifa au kimataifa baina ya wazungumzaji wake.

Licha ya maandiko mbalimbali kuangazia matumizi ya Kiswahili nchini Tanzania na nje ya nchi kubainisha kwamba matumizi ya lugha hiyo yameongezeka, bado uchunguzi zaidi unahitajika ili kubainisha kwa uwazi zaidi nafasi ya Kiswahili katika nyanja mahususi kama vile kazini, kwenye siasa, kwenye huduma za afya na kadhalika ili kuepuka hoja jumuiifu zisizotoa picha halisi kwa wadau na watunga sera za lugha nchini. Hivyo basi, makala haya yanaangazia matokeo ya utafiti wa awali kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika utoaji na upokeaji wa huduma za afya.

¹ Nchini Tanzania, lugha ya Kiingereza inatumika kama lugha ya kufundishia katika elimu ya msingi kwenye shule za watu au mashirika binafsi.

² Awali, Taasisi hii ilijulikana kama Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Mbinu za Utafiti

Data ya makala haya imekusanywa kwa kipindi cha miezi mitatu (3) jijini Dar es Salaam. Nikiwa mkazi wa jiji hili nimekuwa nikitembelea taasisi mbalimbali za afya zikiwemo Kituo cha Afya (KA) cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hospitali ya Temeke (TMK) na hospitali ya taifa ya Muhimbili (MBL). Kwa hiyo, data ya utafiti huu wa awali imekusanywa katika maeneo haya kwa mbinu ya usampulishaji nasibu uliohusisha mahojiano ya ana kwa ana baina ya mtafiti na watoa taarifa. Data hiyo ilirekodiwa katika kinasasauti. Watoa taarifa waliohusishwa ni pamoja na madaktari, wauguzi na wapokeaji wa huduma za afya. Jumla ya watoa taarifa waliohusishwa ni 60. Mchanganuo wa sampuli hiyo ni kama inavyoonekana katika Jedwali namba 1.

Jedwali 1: Mchanganuo wa Watoa Taarifa Walioshiriki

	Madaktari	Wauguzi	Wapokeaji wa huduma za afya
KA	05	05	10
TMK	05	05	10
MBL	05	05	10
JUMLA	15	15	30
JUMLA KUU			60

Nafasi ya Kiswahili katika Utoaji wa Huduma za Afya

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Tanzania na hutumika sambamba na lugha ya Kiingereza katika shughuli mbalimbali za kiofisi. Lugha hii hutumika kama lugha ya kufundishia katika ngazi ya elimu ya msingi hususani katika shule za serikali. Lugha ya Kiswahili hufundishwa kama somo katika elimu ya sekondari na vyuoni ilhali lugha ya Kiingereza ikitumika kama lugha ya kufundishia katika ngazi hizo. Hivyo, wataalamu wa afya kama walivyo wataalamu wa kada zingine, hujifunza kwa lugha ya Kiingereza. Wataalamu hawa husoma vitabu, majarida na maandiko mengine yaliyoandikwa kwa Kiingereza. Kwa hiyo, wataalamu wa afya hupata ujuzi wao kwa lugha ya Kiingereza na kwa sehemu ndogo lugha ya Kilatini³. Kutokana na hali hiyo, wataalamu hawa huwa na uwezo zaidi wa kutumia ujuzi wao na kuufafanua ujuzi huo kwa kutumia lugha ya Kiingereza lakini hufanya mawasiliano ya kawaida kwa lugha ya Kiswahili. Wataalamu hao hulazimika kutumia lugha mbili (Kiswahili na Kiingereza) wakati wa kutoa huduma kutokana na ukweli kwamba watu wengi wa jamii wanayoihudumia huzungumza lugha ya Kiswahili. Suala

³ Majina mengi ya madawa na tiba hutokana na lugha ya Kilatini.

hili limebainika wakati wa utafiti huu wa awali baada ya kuona kwamba jumla ya wapokeaji wa huduma za afya waliohojiwa (30) katika hospitali ya Muhimbili, Temeke na Kituo cha Afya ambapo wapokeaji wa huduma za afya 7 (23%) ndio waliokuwa na uwezo wa kuzungumza Kiingereza kwa kiasi fulani kama jedwali lifuatalo linavyonyesha:

Jedwali 2: Matumizi ya Kiswahili kwa Wapokeaji wa Huduma za Afya Nchini Tanzania

LUGHA	MBL	TMK	KA	JUMLA KUU
Kiswahili	07	09	07	30
Kingereza	03	01	03	
JUMLA	10	10	10	

Katika hali hii ni wazi kwamba wapokeaji wa huduma (wapokeaji wa huduma za afya) wengi hawajui lugha ya Kingereza, lugha ambayo wataalamu wa afya hulazimika kuitumia kutokana na kupata mafunzo ya utaalumu wao kwa lugha hiyo. Katika mazingira haya matumizi ya lugha katika uwanja huu wa afya yanahitaji kuchunguzwa ili kubaini ni kwa kiasi gani lugha ya Kiswahili inatumika na ni changamoto zipi zinawakabili watoaji na wapokeaji wa huduma ya afya wanapotumia lugha hiyo. Matokeo ya uchunguzi wa awali uliofanywa yamewasilishwa katika makala haya kwa kugawanywa katika vipengele vikuu vinne. Vipengele hivyo, vimefafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

Matumizi ya Kiswahili katika Mahojiano baina ya Mgonjwa na Daktari

Katika utafiti huu wa awali, imebainika kwamba mahojiano ya daktari na mgonjwa hufanywa kwa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, matokeo yanaonesha kwamba mazungumzo hufanywa kwa lugha ya Kiswahili lakini mahojiano hayo huandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Kwa hiyo, mahojiano kuhusu hali ya mgonjwa na jinsi anavyojisikia hufanywa kwa lugha ya Kiswahili kisha kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Aidha, majina ya baadhi ya magonjwa hurejelewa kwa lugha ya Kilatini. Yafuatayo ni maelezo ya mgonjwa yaliyotafsiriwa na daktari husika:

Kielelezo 1: Maelezo ya Mgonjwa⁴ Yaliyotafsiriwa na Daktari kwa Kingereza

MINISTRY OF HEALTH - TANZANIA
 MUHIMBILI NATIONAL HOSPITAL
 P.O. Box 65000
 DAR ES SALAAM
 Phone 2151599

Clinical Notes
 Hospital reg. Number _____ Sheet No. MO2-59-47

Address _____

Doctor incharge of firm, name _____ Date of Birth 1/7/22 Sex F

Hypersensitivity, special observation _____ Religion _____ Clinic/ward _____

Notes	
Date (day, month, year) and time	Notes (History, Physical examination, diagnosis, investigation, treatment etc) Each entry should be dated and bear name and signature of the doctor
04/8/2026	Seen pt Admitted from Clinic. 1 1/2 yr female from Kumbuni
Interview - Mother	Known Nephrotic Syndrome for past 2 months Dx at MNH. On regular Prednisolone and Omeprazole. 2 months ago was admitted due to Eye swelling diarrhoea and abdominal distension.
	Cl - Oral lesion 1/2 - Paecil and LL oedema 3/4
	Child was well till 1 month ago when her mother noticed a whitish lesion on the mouth which started on the inside of the tongue and spread to involve a whole finger and finally gums which easily removed by finger. There were no feeding disturbances. No H/o of bleeding per oral. Pt has history of passing loose stool at least twice a day, no blood in the stool. History of refusing to eat. No the vomiting. Pt has a history of fever for 2 weeks ago especially on night hours on and off which improved by taking paracetamol. 2 days ago she has no episode of fever. 2 weeks ago the child developed a gradual onset of body swelling started on the

Muhimbili National Hospital Form No. A-005

Kama inavyoonekana katika mfano wa 1 hapo juu, lugha ya Kiingereza imetumika katika maandishi yaliyotokana na mazungumzo baina ya daktari na mgonjwa yaliyofanywa kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo, ni wazi kuwa lugha ya Kiswahili inatumika katika mazungumzo pekee. Kwa mujibu wa wahudumu waliohojiwa kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili, walieleza kwamba lugha ya Kiingereza ndiyo lugha ya kitaalamu. Ilibainishwa kuwa ni vigumu kwao kutumia lugha ya Kiswahili kuandaa taarifa za kimatibabu kwa sababu walipata

⁴ Kwa kuzingatia itikeli za utafiti, baadhi ya taarifa katika kielelezo hiki kama vile majina ya wapokeaji wa huduma za afya husika na taarifa nyingine zinazohitaji usiri zimeondolewa.

taaluma zao kwa lugha ya Kiingereza. Hivyo, mara nyingi wanashindwa kupata istilahi za Kiswahili zinazoendana na taaluma yao.

Matumizi ya Kiswahili katika Uwasilishaji wa Vipimo na Majibu ya Vipimo
Matokeo kuhusu matumizi ya Kiswahili katika uwasilishaji wa vipimo na majibu ya vipimo yanaonekana kufanywa kwa lugha mbili, yaani Kingereza na Kiswahili. Kwa kawaida, vipimo na majibu ya vipimo husika huwa ni siri ya mgonjwa na daktari au muuguzi husika. Matokeo ya makala haya yamebaini kwamba maelekezo ya vipimo hutolewa kwa mgonjwa kwa mazungumzo kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, maelekezo hayo huandikwa na daktari kwa lugha ya Kingereza. Katika maeneo yaliyofanyiwa utafiti ilibainika kuwa maelekezo ya vipimo huandaliwa katika fomu maalumu ambayo hutolewa kwa mgonjwa kwa kuwekewa alama za nyota, pata au kuzungushia kipimo husika ili kubainisha vipimo maalumu vinavyohitajika kwa mgonjwa anayehusika. Aidha, ilibainika kwamba fomu hizo huandaliwa kwa lugha kienzo ya Kiingereza ingawa maelekezo hayo hutafsiriwa na daktari au muuguzi wakati wa kumpa mgonjwa maelekezo. Kielezo kifuatacho kinaonesha mfano wa fomu maalumu ya maelekezo ya vipimo:

Kielelezo 2: Fomu⁵ Maalumu ya Vipimo

UHC FN° 1

UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM
HEALTH CENTRE
P. o. Box 35074; Tel: 2410014
LABORATORY INVESTIGATION FORM

CLINICAL DIAGNOSIS					
1. _____					
2. _____					
3. _____					
Patient's Name: _____ Date: _____					
HAEMATOLOGY			BLOOD CHEMISTRY		
Test	Results	Normal Range	Test	Results	Normal Range
BS for MPS			FBG		3.9- 6.1 mmol/l
Hb g/dl		M:13-17 / F:12-15	RBG		3.9-7.8 mmol/l
PCV %		35 - 47 %	2HPP		mmol/l
TWBCs		4,000- 11,000 /Cu.mm	Urea/BUN		10 - 45 mg/dl
Differential Count			Creatinine		0.7 - 1.2 mg/dl
Neutrophils		45-75 %	Na+		135 -145 mmol/L
Lymphocytes		20-45 %	K+		3.5 -5.0 mmol/L
Monocytes		5-10 %	Ca++		8.5 - 10.5 mg/dl
Eosinophils		3-6 %	Uric Acid		< 7.0 mg/dl
Basophils		0-1 %	Cholesterol		< 200 mg/dl
Band			T.G		< 190 mg/dl
Blast			LDL		< 160 mg/dl
Nucl. RBCs			HDL		< 55 mg/dl
RBCs count		4.5-5.5 mil/cu.mm	Total Protein		6 - 8 g/dl
MCV		79-92fL	Albumin		3.5 - 5.0 g/dl
MCH		26-33.SPG	Bilirubin (T)		1.1 mg/dl
MCHC		27-32g/dl	Bilirubin (D)		0.3 mg/dl
Retics Count		0.5 - 1.5 %	ALP		73 - 207 U/L
Platelets count		150-450x1000/Cumm	SGOT/AST		< 40 U/L
Blood Group & Rh Factor			SGPT/ALT		< 40 U/L
ESR		< 20 mm/Hr	GGT		< 66 U/L
SEROLOGY					
Widal Enterica			HbsAg		
S. typhi-O		< 1/80	HCV		
S.paratyphi-OB		< 1/80	VDRL		
S.typhi-H		< 1/80	HIV		
A.S.O titre		< 200 IU/ML	RF		< 8 IU/ML
URINE ANALYSIS			STOOL ANALYSIS		
Macro- Examination		Micro-Examination /HPF	Macro-Exam-		
Color		Pus cells	Consistency		
P.H		RBCs	Color		
S.G		Epith cells	Mucus		
Sugar		Crystals	Blood		
Ketone		Cast	Reaction		
Protein		Ova	Worms		
Bilirubin		Yeast cells	Undigested Food		
Urobilinogen		Others	Micro- Exam /HPF		
OTHER INVESTIGATIONS					
UPT			Pus cells		
HVS			RBCs		
Urethral swab			Ova		
Urine C/S			Trophozoite		
			Cyst		
			Others		

Medical Lab. Technician _____ Date _____

Chanzo: Uwandani – Kituo cha Afya – Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Kama ilivyo kwenye fomu ya vipimo, majibu ya vipimo huwasilishwa kwa maandishi kwa lugha ya Kiingereza. Ripoti huandikwa kwa Kingereza ilhali daktari hutafsiri ripoti hiyo kwa Kiswahili wakati wa kuiwasilisha kwa mgonjwa

⁵ Kwa kuzingatia itikeli za kiutafiti baadhi ya taarifa zilizoandikwa katika fomu hii kama vile majina ya wagonjwa na wahudumu wa afya yamefichwa.

wake. Katika mazingira haya ni wazi kwamba taaluma ya tafsiri inachukuliwa kama kipaji maalumu walichonacho watoa huduma za afya. Kwamba ni tafsiri ipi huzingatiwa wakati wa kutoa huduma ni suala linalohitaji kuchunguzwa kwa kina. Suala la kuzingatia ni kwamba watoa huduma za afya hupata taaluma zao kwa Kingereza lakini huhitaji kutumia Kiswahili ili kufanikisha mawasiliano kati yao na wateja wao. Hivyo basi, katika uwasilishaji wa vipimo na majibu ya vipimo, Kiswahili hutumika katika mazungumzo baina ya daktari au muuguzi na mgonjwa pekee ilhali Kingereza kikitumika katika maandishi ya vipimo na ripoti zote za majibu ya vipimo. Kielelezo kifuatacho ni mfano wa ripoti ya vipimo iliyoandikwa kwa lugha ya Kingereza:

Kielelezo 3: Mfano wa Ripoti Iliyoandaliwa kwa Lugha ya Kingereza

Booked (18/8/2016)

Muhimbili National Hospital - Central Pathology Laboratory
Mindu Street, Ijala District, P.O. Box 65002, Dar es Salaam
Fax: +255 2221 50534
Report Form

Barcode: 010 40010 010 010010
PAC: 010 40010 010 010010
MKN: 010 40010 010 010010

Name: _____ Age 13^{1/2} Sex F
Phone No. MC 4-94-30 Address _____ Occupation _____
Contact # _____ Ward/Clinic 36 Date 16/8 Time PM
Clinical History Hemangioma / Lymphangioma
Specimen cc 16/8 Time PM
Specimen ref 16/8 Time 2:12
Sample type Blood Condition when received Good
Sample Unique I.D. _____ Priority: Urgent Routine

*130
16*

For clinical use
Has patient previously been transfused? Yes No Any known transfusion reaction? Yes No
Patient blood group if known: _____
Investigations required: ABO & Rhesus grouping Direct Coombs Indirect Coombs Haemolysin test X-match Transfusion Reaction
Blood or blood product required: Whole blood Packed redcells Fresh frozen plasma Platelet concentrate
No. of units required 60 mls.

For laboratory use only
(Results for ABO & Rhesus grouping, Direct/Indirect Coombs test, Haemolysin test)

ABO & Rhesus grouping	O POS	Direct Coombs	_____
Indirect C	_____	Haemolysin test	_____
Performed	Date 16/08/2016 Time 23:00		
Verified I	Date 16/08/2016 Time 23:00		

For laboratory use: (Results for X-match)

Unit No.	Patient ABO & Rh group	Donor ABO & Rh group	BT Number	Date & Time of X-match		Compatibility	Performed by	Verified by
				Date	Time			
✓ 2278	O POS	O POS	1149	17/08	1:35	Comp	Musse	
✓ 2295	O POS	O POS	13018	17/8	11:16	Comp	Kandari	
✓ 11900186	O POS	O POS	134318	19/8	1:10	Comp	Sakari	

17/8/16. Please issue more blood 60 mls of whole blood urgently

Note: This is a controlled document. Photocopying is prohibited without prior approval from the Quality Officer
CPL MNH CPL TF 041 Version 02- March 2013 Page 1 of 1


19/8/16 please issue more blood 60 mls of whole blood urgently

Matumizi ya Kiswahili katika Maelekezo kuhusu Matumizi ya Dawa

Kipengele hiki kinaangazia maelekezo ya matumizi ya dawa yatolewayo na daktari au muuguzi na yale ambayo huandikwa ama juu ya dawa yenyewe au kwenye karatasi iliyoko ndani ya boksi la dawa. Kutokana na matokeo ya utafiti huu wa awali, imebainika kwamba daktari au muuguzi hutoa maelekezo kwa mgonjwa kwa njia ya mazungumzo kuhusu jinsi ya kutumia dawa kwa lugha ya Kiswahili. Maelekezo hayo huandikwa kwa lugha ya Kiingereza kama kielelezo kifuatacho kinavyoonesha:

Kielelezo 4: Maelekezo kuhusu Matumizi ya Dawa


2.

 **MUHIMBILI NATIONAL HOSPITAL**
P.O. BOX 65000, DAR ES SALAAM

No: **211**

Hospital:
 Patient:
 Address:
 Age: **1768** Sex: **M** Wt:
 Ward/Clinic: **02** Diagnosis:

For medical use only	Pharmacy use only		
	Item prescribed	Amount	Tshs
Rx	T. ASA 75y (min) bd 1/2		
	↑. Paracetamol 40y bd 1/2		
	T. Arbutin 20y nocte x 1/2		
	↑. N. kelip 20y bd 1/2		
	W NS → 10.5 / 24h		
Total Cost			

Signature: 

Code No. **11/123** Date: **6/7**
 Dispensed by: Date: **6/7**

Hata hivyo, imebainika kwamba zipo dawa chache sana zenye majina ya Kiswahili. Huenda hali hii hutokana na ukweli kwamba dawa nyingi hutengenezwa nje ya Afrika. Matokeo ya utafiti huu wa awali yamebaini dawa za aina tatu zenye majina ya Kiswahili kama yanavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 3: Mifano ya Majina ya Dawa Yanayotokana na Lugha ya Kiswahili

Na.	Jina la Dawa	Kazi	Mahali Ilipotengenezwa
1.	Dawa tatu	Inatibu maumivu	Kenya
2.	Dawa ya mba	Inatibu mba	Tanzania
3.	Familia	Dawa ya uzazi wa mpango	Afrika Kusini

Data katika jedwali hili inadhihirisha kwamba licha ya baadhi ya dawa kutengenezwa nje ya Tanzania, majina yake yanatokana na lugha ya Kiswahili kama inavyoonekana katika mfano namba 1 na mfano namba 3.

Matumizi ya Kiswahili katika Maelekezo mbalimbali na Matangazo kuhusu Huduma za Afya

Matokeo ya utafiti huu wa awali yanaonesha kwamba baadhi ya maelekezo na matangazo huandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, baadhi ya maelekezo na matangazo huandikwa ama kwa Kiingereza au kwa Kiswahili na Kiingereza. Imebainika kwamba vipaperushi vingi vilivyochunguzwa viliandikwa kwa Kiswahili. Tazama mfano wa kipeperushi kifuatacho:

Kielelezo 5: Mfano wa Kipeperushi Kilichoandaliwa kwa Kiswahili

Ni muhimu

- Mtoto aanze kunyonya ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa
- Mtoto anyonyeshwe maziwa ya mama ya mwanzo yenye rangi ya njano (colostrum)
- Mtoto anyonyeshwe kila wakati usiku na mchana
- Mtoto aendelee kunyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila hata maji katika miezi sita ya mwanzo

Kumbuka...

- Maziwa ya mama yana maji na virutubishi vyote anavyohitaji mtoto katika miezi sita ya mwanzo kwa afya na ukuaji bora
- Mama anaweza kukamua maziwa yake na mtoto kulishwa wakati mama anapokuwa mbali na mtoto wake.



WATOA HUDUMA ZA AFYA

Kunyonyesha ndani ya saa moja baada ya mama kujifungua huanzisha utengenezaji na utokaji wa maziwa ya mama.

Watoa huduma za afya tunaowajibu wa kumsaidia mama kuanza kunyonyesha katika saa moja ya mwanzo.



Chanzo: Hospitali ya Temeke

Aidha, vipeperushi kuhusu lishe, uzazi wa mpango na matangazo vimetumia lugha ya Kiswahili wakati maelekezo katika baadhi ya ofisi na vyumba vya kutolea huduma mbalimbali hutumia zaidi lugha ya Kingereza. Hivyo basi, maneno kama “injection room” ikiwa na maana ya “chumba cha sindano” na “laboratory” ikiwa na maana ya “mahabara” yalionekana katika baadhi ya ofisi husika katika baadhi ya vituo vilivyofanyiwa utafiti. Wakati mwingine, lugha zote mbili zilitumika ambapo maneno mawili ya lugha mbili tofauti yalitenganishwa kwa kutumia mstari wa mshazali kama vile “washroom/choo”. Kwa jumla, matumizi ya Kiswahili katika maelekezo na matangazo yalikuwa kama ifuatavyo:

Jedwali 4: Matumizi ya Kiswahili katika Maelekezo na Matangazo Kuhusu Huduma za Afya

Lugha	Vipeperushi	Matangazo	Maelekezo	Jumla	Asilimia
Kiswahili	08	06	07	21	61.7
Kingereza	01	02	-	03	8.8
Kiswahili na Kingereza	-	-	05	05	14.7
Lugha zingine	-	-	03	03	8.8

Kama inavyoonekana katika jedwali namba 4, maelekezo na matangazo kuhusu huduma za afya yanaonekana kutumia lugha ya Kiswahili kwa asilimia 61.7. Aidha, lugha ya Kiingereza imetumika kwa asilimia 8.8 hususani kwenye matangazo na vipeperushi. Watoa taarifa waliohusishwa walieleza kwamba baadhi ya maelekezo muhimu yaliandaliwa kwa lugha ya Kiingereza kwa sababu ilidhaniwa kwamba baadhi ya wapokeaji wa huduma walitarajiwa kuwa wageni ambao hawajui lugha ya Kiswahili. Utafiti huu umebaini kwamba wapokeaji wa huduma za afya walielewa vyema lugha ya Kiswahili kwani maelekezo ya Kiswahili yaliwasaidia sana. Ilibainika wazi kwamba waliweza kutaja mahali waendako kwa ujasiri bila kusitasita ilhali mahali ambapo palirejelewa kwa lugha ya Kiingereza wapokeaji wa huduma waliowengi walipata wakati mgumu kutaja waendako. Iliwalazimu kutaja shughuli zinazofanyika katika ofisi au vyumba husika kwa Kiswahili badala ya kutumia maneno kama “labour room” au injection room” na kadhalika. Hali hii ya lugha kuwa kikwazo katika utoaji na upokeaji wa huduma za afya imewahi kuelezwa na Al-Khathami na wenzake (2010). Pamoja na kudokeza suala hilo, anasisitiza kwamba lugha ni nyenzo muhimu katika upatikanaji wa huduma za afya katika jamii yoyote.

Changamoto Zinazowakabili Watanzania Wanapotumia Kiswahili katika Utoaji na Upokeaji wa Huduma za Afya

Utafiti huu wa awali umebaini changamoto mbalimbali zinazowakabili watoaji na wapokeaji wa huduma za afya waapotekeleza majukumu yao ya msingi kwa

kutumia lugha ya Kiswahili. Changamoto hizo ni pamoja na wataalamu kukosa msamiati maalumu wa Kiswahili, matumizi ya lahaja mbalimbali za Kiswahili, matumizi ya lugha za asili, matumizi ya misimu, matumizi ya tafsida na uchanganyaji msimbo. Changamoto hizi zimefafanuliwa katika vipengele vinavyofuata:

Wataalamu wa Afya Kukosa Msamiati Mahususi wa Kiswahili

Uchunguzi huu wa awali umewahusisha madaktari na wauguzi. Data iliyokusanywa inaonesha kwamba wataalamu hawa hawana istilahi za Kiswahili za kutosha zinazohusiana na taaluma ya afya. Suala hili lilielezwa bayana na wataalamu waliohusishwa katika utafiti huu. Ilifafanuliwa kuwa changamoto hii inatokana na wataalamu hao kupata taaluma zao kwa lugha za kigeni hususani Kingereza. Aidha, ilielezwa kuwa wataalamu hawa hujaribu kutumia baadhi ya istilahi za Kiswahili wanazozijua lakini hushindwa kuelewana na watu wanaowahudumia. Hali hii inadhihirisha ukweli kwamba inahitajika juhudi kubwa kuielimisha jamii ya Watanzania kuhusu istilahi mbalimbali za kada mahususi kama vile afya, sheria, siasa na kadhalika.

Matumizi ya Lugha za Asili

Ilifafanuliwa kuwa baadhi ya wapokeaji wa huduma za afya hutumia lugha za asili pekee. Aidha, baadhi yao huzungumza Kiswahili kisichoeleweka. Ilifafanuliwa kwamba hali hii ikijitokeza mtoa huduma hulazimika kutafuta ama mfanyakazi au ndugu wa mgonjwa anayejua lugha husika na lugha ya Kiswahili ili kuweza kurahisisha mawasiliano. Ilielezwa kwamba hali hiyo husababisha kupoteza muda mwingi kumtibu mgonjwa mmoja na wakati mwingine mgonjwa hupoteza maisha kabla ya matibabu. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba kati ya wapokeaji wa huduma kumi (10) waliohusishwa, watatu (3) hawakuweza kuzungumza lugha ya Kiswahili inayoeleweka. Suala hili linaonesha kwamba wadau wa Kiswahili wanatakiwa kuongeza jitihada za kueneza Kiswahili hususani katika maeneo ya pembezoni mwa miji ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanaweza kuzungumza na kuwasiliana kwa Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano baina yao.

Kwa upande mwingine, Barnett (2016) anasisitiza kwamba kwa kawaida mtu yeyote huwa huru kujieleza kwa kutumia lugha mama hasa anapokuwa na msongo wa mawazo au hisia ambazo sio za kawaida kama vile mshtuko. Hii inamaanisha kuwa mpokeaji wa huduma za afya hujieleza vema na kwa uhuru anapotumia lugha mama. Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu ni wazi kwamba baadhi ya wapokea huduma za afya hupendelea kutuma lugha mama ili waweze kujieleza vizuri. Hata hivyo, changamoto inayojitokeza ni kuwepo kwa lugha mama nyingi sana kulingana na wingi wa makabila yaliyopo nchini Tanzania. Kiswahili basi huchukua nafasi ya kuwaunganisha Watanzania ili

kuweza kuwasiliana ingawa siyo Watanzania wote wanaweza kujieleza vyema kwa Kiswahili.

Matumizi ya Lugha za Mitaani

Changamoto nyingine iliyobainishwa ni matumizi ya lugha za mitaani. Nilieleza hapo awali kwamba licha ya wapokea huduma waliowengi kutumia lugha ya Kiswahili inayoeleweka, baadhi yao hutumia lugha za mitaani. Ilifafanuliwa kwamba kundi la vijana hususani wanaotumia madawa ya kulevya hutumia lugha za mitaani suala ambalo husababisha mawasiliano ama kutokukamilika au kukamilika kwa kuchelewa. Mifano ya sentensi ambazo ziliwahi kutumiwa na kushindwa kueleweka kwa watoa huduma za afya ni kama vile “Daktari, nahitaji kucheki afya maana nimeuza mechi mara nyingi sana.” Sentensi hii ilifafanuliwa kuwa ina maana kwamba mpokea huduma aliyetoa sentensi hiyo alimaanisha anahitaji kupima kwa sababu amefanya tendo la ndoa bila kutumia kinga yoyote mara nyingi sana. Sentensi nyingine ni “Daktari naomba ushauri maana naona mwili wangu unakauka taratibu.” Sentensi hii ina maana kwamba mpokea huduma anahitaji ushauri kwa sababu anakonda sana bila sababu. Sentensi nyingine ni kama “Naomba msaada mama anafrashi kwelikweli.” Hii ina maana kwamba mhusika anahitaji msaada kwa sababu mama yake anaharisha sana. Ilisitizwa kwamba matumizi ya sentensi zenye maneno kama haya husababisha watoa huduma kutumia muda mrefu kabla ya kung’amua kusudio la mpokea huduma.

Matumizi ya Lahaja mbalimbali za Kiswahili

Imebainika kwamba changamoto nyingine inayowakabili watoa huduma na wapokeaji wa huduma za afya wanapotumia Kiswahili ni matumizi ya lahaja mbalimbali za Kiswahili. Ilielezwa kwamba baadhi ya maneno yanayotokana na lahaja hizo hayajulikani au wakati mwingine huwa na maana tofauti na ile iliyozoeleka. Katika kushadida hoja hiyo, ilielezwa kuwa baadhi ya maneno kutoka katika lahaja za Kiswahili zinazotumika Zanzibar hutofautiana na yale ya Tanzania Bara. Mfano uliotolewa kuhusu hoja hii ni pamoja na sentensi kama “Ameanza kuharisha baada ya kunywa maji ya mferejini.” Ilielezwa kwamba daktari aliposikia sentensi hiyo kwa mara ya kwanza alidhani mgonjwa husika alikunywa maji ya mtaloni. Hata hivyo, baada ya mhusika kutoa ufafanuzi zaidi ilibainika kwamba mgonjwa alikunywa maji ya bombani. Sentensi nyingine ni kama vile “Alianza kutapika mara tu baada ya kula tungule.” Ilielezwa kuwa daktari alipata taabu sana kuelewa tungule ni nini. Ilifafanuliwa kwamba mpokeaji wa huduma alikusudia kusema kwamba mgonjwa wake alianza kutapika mara baada ya kula nyanya. Kwa hiyo, wakati Tanzania Bara tunatofautisha bomba la maji na mfereji, kwa upande wa Zanzibar bomba hujulikana kama mfereji. Wakati huo huo, kile kinachoitwa nyanya Tanzania Bara, Zanzibar hujulikana kama tungule. Katika mazingira haya, mawasiliano

ama hushindwa kukamilika au hucheleweshwa na kusababisha huduma za afya kucheleweshwa na wakati mwingine wahusika wasipokuwa makini wanaweza kuandaa ripoti zisizosahihi.

Hitimisho

Makala haya yameangazia nafasi ya Kiswahili kwa mwelekeo wa mawanda mahususi kwa lengo la kubainisha na kujadili nafasi ya Kiswahili katika utoaji wa huduma za afya nchini Tanzania. Licha ya ukweli kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha inayofahamika sana kwa Watanzania waliowengi, makala haya yamebainisha changamoto mbalimbali zinazowakabili Watanzania wanapotumia lugha ya Kiswahili wakati wa kutoa au kupokea huduma za afya nchini. Imabainika kuwa katika utoaji na upokeaji wa huduma za afya, lugha ya Kiswahili hutumika kwa kiasi kikubwa kwenye mazungumzo ilhali nyaraka mbalimbali zikiandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Ilikelewa kuwa hali hii hutokanana wataalamu wa afya kupata mafunzo kwa lugha za kigeni suala linalosababisha wataalamu hao kukosa msamiati wa kitaalamu wa lugha ya Kiswahili. Aidha, changamoto mbalimbali zilizobainishwa na watoa taarifa ni pamoja na matumizi ya lahaja mbalimbali za Kiswahili, kutofautiana kwa lugha mama na tamaduni za lugha husika matumizi ya misimu au lugha za mitaani, matumizi ya lugha za jamii⁶. Kutokana na changamoto hizi, lugha ya Kiswahili hushindwa kutumika kikamilifu katika mawasiliano baina ya watoaji na wapokeaji wa huduma za afya. Hali hii inadhihirisha ukweli kwamba inahitajika juhudi kubwa kwa wadau wa Kiswahili, jamii na serikali kuielimisha jamii ya Watanzania kuhusu istilahi mbalimbali za kada mahususi kama vile afya, sheria, siasa na kadhalika ili kurahisisha mawasiliano na utekelezaji wa majukumu husika kwa wakati na kwa ufanisi.

Marejeleo

- Al-Khathami A. M, Kojan S. W, Aljumah M. A, Alqahtani H, Alrwaili H (2010). "The effect of nurse-patient language barrier on patients' satisfaction." Katika Jarida la *Saudi Medical*. Namba 31, Kurasa 1355-1358.
- Barnett, J. P. (2016). *Analysis of Healthcare Infrastructure and Accessibility for a Minority Population*. Marekani: Shippensburg University.
- Habwe, J. (2009). "The Role of Kiswahili in the Intergration of East Africa". Katika Jarida la *The Journal of Pan African Studies*. Juz. 2 Na. 8. Kur. 2 – 10.

⁶ Lugha za jamii zimefasiliwa kama lugha za asili za makabila mbalimbali kama vile Kikurya, Kisukuma, Kikinga na kadhalika.

- King'ei, K. (1999). "Swahili Technical Terminology: Problems of Development and Usage in Kenya". Makala iliyowasilishwa katika Kongamano la 12 la Swahili Colloquium, Bayreuth, Germany. Kur. 147-160.
- Mazrui, A. A. na Mazrui, A. M. (1995). *Swahili State and Society*. London: James Currey.
- Moshi, L. (2006). The Globalised World Languages: The Case of Kiswahili. Katika Olaoba, F. Arasanyin na Michael, A. Pemberton (wahariri), Selected Proceedings of the 36th Annual Conference on African Linguistics, Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. Kur. 166 – 175.
- Mukuthuria, M. (2006). "Kiswahili and Its Expanding Roles of Development in East Africa Cooperation: A Case of Uganda". Katika Nordic Journal of African Studies. Vol. 15, Na. 2. Kur. 154 – 165.

